

KISWAHILI KARATASI 3

KAGONDO SECONDARY SCHOOL

KCSE Post Trial Exam

Fasihi

September 2015

Saa 2½

**1. Swali la lazima. Tamthilia ya Mstahiki Meya Timothy M. Arege**

*“Nasikia tu! Si vyombo vya habari si wanasiasa, si wasomi.*

- i. Fafanua muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
- ii. Eleza tamathali za usemi zilizotumiwa katika dondoo hili (Alama 4)
- iii. Fafanua sifa tatu za msemaji (Alama 6)
- iv. Msemaji na msemewa wanafafanua baadhi ya matatizo ya wanacheneo. Yataje na ufafanue sita (Alama 6)

**2. Ken Walibora: Kidagaa Kimemwozea**

*“... Alisimama jadidi na kuwatazama hawa watu wawili...”*

- a) Eleza muktadha wa dondoo hii. (Alama 4)
- b) Eleza hulka ya yule *“alisimama jadidi na kuwatazama hawa watu wawili.”* (Alama 6)
- c) Jadili mchango wa wanawake katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea (Alama 10)

3. Huku ukirejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea, eleza jinsi mwandishi amefaulu kutumia mbinu zifuatazo:

- i) Majazi (alama 10)
- ii) Jazanda (alama 10)

**4, HADITHI FUPI**

**Ken Walibora na S. M. Mohamed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.**

*“Mimi nani? Mja nisiye na shukrani. Nisiyefadhilika au nisiyehisi. Mja wa laana, mbwa miye, mi..mi..mi..e.”*

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  
- b) Taja na utoe mfano wa mbinu mbili za fasihi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
  
- c) Eleza hali ya mzungumzaji kama inavyodhihirika katika dondoo hili. (alama 2)
  
- d) “Ulevi una madhara chungu nzima katika jamii.” Thibitisha kwa kurejelea hadithi husika. (alama 10)

5. Fikirini anakumbana na ubaguzi wa aina tofoauti huko *“Ughaibuni”* Dhibitisha kauli hii? (alama 20)

6. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali

Linatushagaza, twashangaa dhidi ya kushangaa!

Kwa maangamizi ya kila leo.

Tunayotekelezewa na kiumbe razini zaidi,

Binadamu!

Hatujui sababu,

Mzinga na mazega yetu kuteketezwa,

Yetu asali kurinwa kwa mababu na waritimba,

Binadamu wasiojua madhila yetu,

Kudamka kutafuta nekta, na kukesha kulinda mzinga!

Lakini kinachotushangaza, twauliwa: Mwatchomeani?

Twafedheka jamani!

Masaibu ya tajiri

Tajiri mwema kuwatajirisha wasio na faida

Badala ya wakatilia moto daraja la fanaka,

Wasijue kesho, kesho kutwa, mtondo...watawuna vipi?

Baada ya kutuamiza, sie vitega chumi vyao.

Tuna haki kama nyinyi,

Ya kuwaona watoto na wetu vijukuuu.

Wakikua na kufaidi, jasho letu wazazio.

Ingawa hili halijawa faradhi,

Ila kwa mapenzi yenu ya dhati.

Kumbuka binadamu,

Hata sisi tuna hisia, tusichomwe,

Japo wajinga tunayo manufaa

Sie hatuwahi, mbona nyie?

Na safari yenu sote, japo njia tofauti.

Twende pole pole!

### Maswali

- a) Eleza dhamira ya mshairi wa utungo huu. (Alama 2)
- b) Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu. (Alama 4)
- c) Taja na utoe mifano miwili ya tamathali za usemi zinazotumiwa katika shairi hili.(Alama 4)
- d) Huku ukitoa mifano mwafaka eleza idhini za utunzi zinazojitokeza katika tungo.  
(Alama 4)
- e) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (Alama 4)
- f) Eleza maana ya maneno yafuatayo , (Alama 2)

i) Razini

ii) Masaibu

### **7. FASIHI SIMULIZI**

- a) Tofautisha na ulinganishe mighani na maghani. (Alama 4)
- b) Huku ukitolea mifano ya kipera husika, fafania dhima nne za maghani. (Alama 8)
- c) Ukifuata utratibu unaokubalika, onyesha hatua sita za uwasilishaji wa vitendawili. (Alam 1)

